JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

Juni, 2023

Dodoma

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS – TAMISEMI

Namba za Simu. 0765509147

Mkuu wa Shule. 0765509147

Makamu Mkuu wa Shule.0625281940

Matron 0764834403

Shule ya Sekondari Malagarasi

S.L.P.. 109

Tarehe ..12/6/2023

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………..............................

S.L.P ……………………………………..

……………………………………..

Yah: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI MALAGARASI HALMASHAURI YA KIBONDO MKOA KIGOMA MWAKA 2023

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2023. na atasoma tahasusi ya ...........


   Shule ya Sekondari Malagarasi ipo umbali wa Kilometa 1.5 Mashariki mwa Mji wa Kibondo, Usafiri wa Tax unapatikana kutoka kituo Cha mabasi Nauli ni Shilingi 5,000 kwa pikipiki na Shilingi 1,000.

   Muhula wa Masomo unaanza tarehe 13/08/2023 hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 13/08/2023 Mwisho wa kuripoti ni tarehe 31/08/2023

2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

2.1 Sare za Shule

i. Sare ya shule hii ni sketi mbili rangi ya damu ya Mzee sketi iwe ndefu ikutane na kiatu ,kitambaa kizito na sio Cha sukari sukari, sketi iwe na marinda ya mkeketo inchi moja na nusu, kwa Wasichana na suruali mbili za rangi ya damu ya Mzee kwa wavulana.

| | | |
|---|---|---|
|  |  |  |
| Rangi ya kijani ya skirt | Rangi ya damu ya mzee ya skirt na suruali za darasani | Rangi ya blue ya t-shirt |

ii. Mashati 2 ya mikono mirefu (Tomato) rangi nyeupe

iii. Rangi ya Hijab (kijuba) ni nyeupe ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama

iv. Sare ya Michezo ni track suti rangi nyeusi yenye mistari(strip ) nyeupe Kwa wasichana na wavulana (pea *moja* ) na kwa wavulana (*pea moja*);

v. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;

vi. Soksi jozi mbili nyeupe za shule;

vii. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali;

viii. Sweta nyeusi yenye shingo ya V kwa mbele (Pia zinapatikana shuleni kwa gharama ya TSH 15,000 kwa watakaohitaji) ;

ix. Nguo za kushindia (*shamba dress*) sketi mbili rangi ya kijana , kijani ya CCM ,sketi iwe na marinda ya mkeketo ya inch moja na nusu iwe ndefu hadi kwenye kiatu.(Pia zinapatikana shuleni kwa watakaohitaji kwa gharama ya Tsh 22,000/)

Pia suruali mbili rangi nyeusi kwa wavulana na T-shirt rangi ya blue ( form six) (Pia t-shirt hizi zinapatikana shuleni kwa watakaohitaji kwa gharama ya TSH 15,000/-)

x. Tai rangi ya damu ya Mzee yenye michirizi nyeupe (Pia tai zinapatikana shuleni kwa gharama ya Tsh 5,000)

xi. Tisheti (T-shirt) ya darasani *Rangi ya kijivu* inapatikana shuleni kwa gharama ya TSH 15,000 *(*T-shirt *moja* );

2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

i. Madaftari tisa ya kaunta book quare 3
ii. Ream (A4) Mbili (2) kwa mwaka aina ya double A;
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika
iv. Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology;
v. Scientific Calculator kwa wanafunzi wanaosoma somo la hisabati (Advanced mathematics na Basic mathematics (BAM);
vi. Godoro linapatikana shuleni kwa kwa kukodi kwa gharama ya TSH 10,000
vii. Mashuka Jozi 2, rangi ya blue blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1 rangi ya blue.
viii. Nguo za ndani za kutosha;
ix. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
x. Ndoo mbili ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;
xi. Kwanja 1, jembe 1, reki 1, mifagio 2 wa ndani soft broom na nje na hard broo au chelewa.

2.3 Michango mbalimbali

a) Shule za Bweni

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | Jumla | 80,000/= |

Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

MUHIMU:

- ❖ Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;

- ❖ Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;

- ❖ Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa).

### 3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;

iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

3. Viambatisho na Fomu Muhimu

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

4. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBU SANA MALAGARASI SEKONDARI

MARTIN KAIZILEGE MATHEW
Mkuu wa Shule

NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -

- Mkuu wa shule...........................0765509147
- Makamu Mkuu wa Shule............0625281940
- Mwandamizi Taaluma…………….0767982120
- Mwandamizi Malezi………………..0759814273

SHULE YA SEKONDARI MALAGARASI
S.L.P 109 KIBONDO, SIMU: 028 2820171
FOMU NAMBA 1 HISTORIA YA MWANAFUNZI

1. Jina la mwanafunzi………………………………………………………………….
2. Jina la baba ……………………………………………………………………………
3. Jina la Mama…………………………………………………………………………..
4. Jina kamili la mlezi…………………………………………………………………..
5. Anuani ya mzazi/mlezi…………………………………………………………
6. Uhusiano wa mlezi……………………………………….........................
7. Kazi ya baba (mkulima, mfanyabiashara, mfanyakazi)…………………………
8. Kama ni mkulima zao muhimu analolitegemea ni………………………………
9. Kama ni mfanyabiashara, biashara yake ni...............................................
10. Kama ni mfanya kazi, kazi yake ni…………………………………………….
11. Afya ya mwanafunzi, kama anayo matatizo ya kiafya na hivyo kustahili huduma maalum. Tafadhali mzazi/mlezi aeleze wazi

    ………………………………………………………………………………,........................

    ……………………….………………………………………………………………………….

    ……………………….………………………………………………….........................
12. Madhehebu ya dini…………………………………………………………..............

13. Jamaa na ndugu wanaoruhusiwa kumtembelea mwanafunzi kwa ruhusa ya mzazi/mlezi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| Jina kamili la | Uhusiano | Namba ya simu | Bandika picha |
| ……………………………… | ……………………………… | ……………………………… | |
| Jina kamili la ndugu | Uhusiano | Uhusiano | Bandika picha |
| ……………………………… | ……………………………… | ……………………………… | |
| Jina kamili la ndugu | Uhusiano | Uhusiano | Bandika picha |
| ……………………………… | ……………………………… | ……………………………… | |
| Jina kamili la ndugu | Uhusiano | Uhusiano | Bandika picha |
| ……………………………… | ……………………………… | ……………………………… | |

SHULE YA SEKONDARI MALAGARASI
S.L.P 109 KIBONDO, SIMU: 0765509147
FOMU NAMBA 2 FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE

Jina la mwanafunzi……………………………………………………………………..................…

Jina la mzazi/mlezi…………………………………………….......................................

Anuani ya .mzazi/mlezi……………………………………………………..................………

Uhusiano…………………………………………… (mjomba, shangazi, kaka, dada).

Mimi………………………………………………………nikiwa nimechaguliwa kuwa mwanafunzi wa Tanzania naamini kuwa nimetunukiwa nafasi hiyo niliyopewa na umma wa Tanzania. Hivyo naahidi kuwa nitajibidiisha kadri ya uwezo wangu wote katika kazi zote nitakazopewa hapa shuleni nje na ndani ya darasa ili kuleta ufanisi. Ili kutimiza shabaha hiyo ninakubali na ninaahidi kwa hiari yangu mwenyewe kuwa nitafanya kazi kwa BUSARA, JUHUDI YA HALI YA JUU KABISA NA UTII kwa viongozi wote wa shule pamoja na sheria. Nikiwa na maoni au malalamiko ninaahidi nitayafikisha panapohusika kwa njia na taratibu zinazokubalika.

Sahihi ya mwanafunzi…………………………….................…..…tarehe……………….........

Mimi ………………………………………………….............………mzazi/mlezi wa mwanafunzi

………………………………………………………..............…………ninaahidi kuwa nitatimiza wajibu wangu kama mzazi/mlezi wa mtoto huyo kwa kushirikiana na shule.

Sahihi ya mzazi/mlezi………………………………………….tarehe……………

MALAGARASI SECONDARY SCHOOL
P.O BOX 109 KIBONDO, TEL: 0765509147
FORM NUMBER 03 MEDICAL EXAMINATION FORM

Pupil’s name…………………………………………………………………………………………………

Age ……………………………………………………………………………………………………………

Stool test……………………………………………………………………………………………………

Blood group…………………………………………………………………………………………………

Urine analysis………………………………………………………………………………………………

Sphills test ……………………………………………………………………………………………………

Chest test……………………………………………………………………………………………………

Speech…………………………………………………………………………………………………………

Eye test ………………………………………………………………………………………………………

Additional information and physical defect or impairment to pursue further studies
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………

Signed by ……………………………………………………………………………

Designation …………………………………………………………………………

Official stump

Date ……………………………